

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA

**MWONGOZO WA BEJI ZA  
WATUMISHI WA UMMA**

**FEBRUARI, 2016**

## **YALIYOMO**

## **KURASA**

1.0	Utangulizi.....	1
2.0	Mambo muhimu kwenye Beji .....	1
2.1	Vipimo vya Beji.....	2
2.2	Nembo .....	2
2.3	Jina la Mtumishi.....	2
2.4	Jina la Taasisi .....	3
2.5	Rangi ya Beji .....	3
2.6	Uvaaji wa Beji.....	3
3.0	Viambatisho.....	3
	Kiambatisho Na. 1 - Taasisi za Umma zinazotumia Nembo ya Taifa pekee.....	3
	Kiambatisho Na. 2 - Taasisi za Umma zinazotumia nembo mbili (Nembo ya Taifa na Nembo ya Taasisi husika).....	4

## VIWANGO VYA BEJI ZA WATUMISHI WA UMMA

### 1.0 Utangulizi

Serikali imekuwa ikiweka viwango mbalimbali vya utendaji kazi kwa dhamira ya kutoa huduma stahiki kwa Umma na kumjali mteja. Azma hiyo imepelekea Serikali kuelekeza kila mtumishi wa Umma kuvaa beji yenye jina lake.

Umuhimu wa kuvaa beji hii ni pamoja na kumpa mteja haki ya kumfahamu mtumishi anayemhudumia na kumrahisishia mteja kufanya ufuatiliaji pale inapohitajika, kutoa mrejesho wa huduma na kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa Umma. Beji pia huongeza usalama mahali pa kazi kwa kusaidia kuwatambua watumishi na wateja/wageni katika eneo la ofisi husika ya Umma.

Kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma imeandaa mwongozo wa viwango vya beji ambavyo vinatakiwa kuzingatiwa na Taasisi zote za Umma. Kwa watumishi ambao sare zao hujumuisha beji zenyе majina yao au aina nyingine za utambulisho utaratibu wa mwongozo huu hautawahu.

### 2.0 Mambo muhimu kwenye Beji

Katika utengenezaji wa Beji, Taasisi za Umma zinatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- i) Vipimo vya beji
- ii) Nembo
- iii) Jina la Mtumishi

- iv) Jina la Taasisi
- v) Rangi ya beji
- vi) Uvaaji

## 2.1 Vipimo vya Beji

Beji inatakiwa kuwa na upana kati ya sentimita 2.0 - 3.0 na urefu kati ya sentimita 7.0 - 8.0.

## 2.2 Nembo

### i) **Taasisi za Umma zinazotumia Nembo ya Taifa pekee**

Nembo ya Taifa iwekwe upande wa kushoto wa beji na iwe na urefu wa 1.2 - 2.002 sentimita na upana wa kati ya sentimita 1.1 - 1.726.

### ii) **Taasisi za Umma zinazotumia nembo mbili (Nembo ya Taifa na Nembo ya Taasisi husika)**

Nembo ya Taifa na ya Taasisi husika zitatumika. Nembo ya Taifa iwekwe upande wa kushoto wa beji na Nembo ya Taasisi iwekwe upande wa kulia wa beji.

## 2.3 Jina la Mtumishi

- i) Jina la mtumishi liwe kwa mujibu wa nyaraka za ajira yake;
- ii) Jina la mtumishi liandikwe kwa herufi kubwa;
- iii) Ukubwa wa fonti usipungue 16;
- iv) Maandishi yawe ya wino mzito unaosomeka kwa urahisi; na
- v) Kwa taasisi zinazotumia nembo moja, jina la mtumishi liwekwe upande wa kulia wa nembo na kwa Taasisi zinazotumia nembo mbili, jina la mtumishi liwekwe katikati ya nembo ya Taifa na Nembo ya Taasisi

## **2.4 Jina la Taasisi**

- i) Jina la Taasisi litakuwa kwa mujibu wa nyaraka zilizounda Ofisi ya Serikali husika;
- ii) Jina la Taasisi liandikwe kwa herufi ndogo;
- iii) Ukubwa wa fonti usipungue 14; na
- iv) Maandishi yawe ya wino mzito .

## **2.5 Rangi ya Beji**

Beji ziwe na rangi yoyote itakayowezesha maandishi kusomeka vema na Nembo kuonekana

## **2.6 Uvaaji wa Beji**

Beji ivaliwe kifuani upande wa kushoto.

## **3.0 Viambatisho**

**Kiambatisho Na. 1 - Taasisi za Umma zinazotumia Nembo ya Taifa pekee**



**Kiambatisho Na. 2 - Taasisi za Umma zinazotumia nembo mbili  
(Nembo ya Taifa na Nembo ya Taasisi husika)**

